



**NINI
HUTENDEKA
BAADA YA
KIFO?**

**UJUMBE MUHIMU
UTAKAOWEZA
KUSOMA**

ukweli: Hivi karibuni utakufa.

Kila mahali duniani kuna kaburi linalotoa ushahidiwa kwamba **maisha yako hivi karibuni yatafikia mwisho**. Je, U tayari? Ni kitafanyika baada ya kifo chako?



Baada ya kifo chako

Waweza kuamini ya kuwa:

- *Utaenda mbinguni au kuzimu*
- *Kuingia ulimwengu wa kiroho*
- *Kurejea tena ukiwa mnyama au mtu
mwingine*
- *kuacha kuwapo*

au

- *Hujui nini cha kuamini*



ULIMWENGU MMOJA - DINI NYINGI

Kwa kadri kuna dini 4,200. Hizo ni dini nyingi sana!

Katika Kenya peke yake, kuna miundo tofauti ya ukristo, uislamu, ubhai, ubudhana uhindi.

Pia kuna makabila 42 hapa Kenya na kila kabilia liko na mila zake za kidini.

Dini 4,200 - na zinafundisha kitu tofauti namna tulivyopatikana hapa, kusudi letu ni gani na ni nini hutendeka tunapokufa.

Na nwa kuwa wanafunza kitu tofauti....

Zote haziwezi kuwa kweli!



Ni rahisi kuchanganyikiwa panapo dini nyingi



NA MILELE NI MUDA MREFU WA KUFANYA KOSA

Kwa hivyo Kutokana na hizi dini zote...

Imani ya Kikristo
Imani ya
kiukabilalmani
ya Ubahai Imani
ya Kiislamu
Ubudha
Uhindu



Ipi iliyo kweli?

**Kwa kuwa Mungu wa pekee na kweli anatupenda,
ametupa neno lake ili tuweze kujua kwamba...**

1. Maisha yako yana maana ya milele na kusudi!
2. Kuna tumaini zaidi ya kaburi!
3. Unapendwa na muumba wako!
4. Utawajibika mbele ya Muumba wako!

Kijitabu hiki kitakuwezesha kujifunza kumhusuMungu na Neno lake ili uweze kujua namna ya kutimiza kusudi lako duniani, uwe na ushindi dhidi ya kaburi na ukubalike na Mungu utakapokufa. Ustawi wako wa milele u hatarini **na umilele haukosei!**

Mungu amenena na mwanadamu

limwengu huu umejaa dini za kibinadamu zisizokubaliana na zinategemea itikadi za wanadamu. Hali ndiyo hiyo na njia ya pekee ya kujua ukweli ku-husu Mungu ni kama tutamsikiliza **Mungu** mwenyewe. Hi ndio maana tunafaa kutegemea rekodi iliyohamasishwa (mwongozo wa Mungu) na si kufuata mawazo ya Mwandamu.


**Kila andiko
lenye pumzi
ya Mungu.**

2 Timotheo 3:16

Mungu amenena na mwanadamu

Biblia ya Kiyahudi, (pia inajulikana kama torati Agano la kale,nk). Ni kitabu asili kinachoonyesha kwamba **Mungu ndiye mwandishi.**

Kila maandishi mengine "matakatifu" yanategemea juu ya Biblia hii ya Kiyahudi.*



*Uhindu na imani ya Wabahai ni mchanganyiko wa dini zote, kwa hivyo ha-ziongozwi na Mungu na hazijumuishwi.

Kitabu Kimoja – Dini Nyingi

Kutokana na hiki kitabu kimoja ambacho ni Biblia ya Kiyahudi kulitokezea kila dini kubwa → kubwa (zinazomwamini Mungu Mmoja wa kweli aliyejifunua mwenyewe kwa mwandamu).

- ✓ Ukristo
- ✓ Uyahudi
- ✓ Ukatoliki
- ✓ Uisilamu
- ✓ Umormoni
- ✓ Mashahidi wa Yehova

Changamoto ni kuwa licha ya kwamba dini zote kuu zilitokana na kitabu kimoja, mafundisho yao yanatofautiana. Ni jinsi gani tutakavyojua iliyo kweli? Tunaweza kujuaukweli kwa kujua ujumbe halisi wa Mungu kutoka kwa Agano la Kale!

Jambo la kimsingi ni kuelewa agano la kale

***Kuelewa agano la kale ndio msingi
wa kujua ukwelijuu ya Mungu,
uzima na kifo.***



**Tuangalieni mambo 8 ya kimsingi yanayoyafundisha:
KWANZA:**

Mungu ni wa MILELE—Mungu hana mwanzo wala mwisho “*...Tangu milele hadi milele wewe ni Mungu*” (Zaburi 90:2).

Mungu ni Roho—“***Mungu ni Roho...***” (Yohana 4:24).

Mungu ni Mkamilifu—“***Wewe U mwema na unafanya mema***” (Zaburi 119:68).

Kuelewa Agano la Kale...

PILI: Hapo mwanzo Mungu aliumba dunia, anga, anga ya juu na kila kitu kilichomo. Kwa kuwa Mungu ni mkamilifu kila kitu Mungu aliumba kilikuwa bora. Mungu aliumba binadamu (Adamu), ambapo kutoka-na naye watu wote waliweza kuzaliwa. Naye Mungu alimpenda mwanadamu sana.



“Na Mungu aliona kila kitu alichokifanya, na tazama ni chema sana” (Mwanzo 1:31).

Kuelewa Agano la Kale...

TATU: Mungu aliumba binadamu kwa mfano wake.

“Naye Mungu akasema, na tumfanye binadamu kwa mfano wetu, kwa sura yetu...” (Mwanzo 1:26).

Ona kwamba Mungu alisema "**tumfanye.**" Mungu ni Mungu mmoja aliye utatu: 1) Mungu Baba, 2) Mungu Mwana, na 3) Mungu Roho Mta-katifu. Mungu si miungu watatu; Yeye ni Mungu mmoja kwa utatu. Mungu ni utatu (utatu wa Mungu).

“Bwana Mungu wetu ni Bwana Mmoja...” (Kumbukumbu laTorati 6:4b).

“Mimi ni Bwana, wala hapana mwengine zaidi yangu, zaidiyangu hapana Mungu....” (Isaya 45:5).

Kuelewa Agano la Kale...

Kwa kuwa Mungu ni Roho Alitupa roho kutuwezesha kumjua na kumwabudu.

“Mungu ni roho na wote wanaomwabudu inawapasa wamwabudu katika roho ...” (Yohana 4:24).

Mungu alipeana:

Mimea—**Mwili** (kuishi na kukua)

Wanyama—mwili na **nafsi** (Kujitambua)

Binadamu—Mwili, nafsi na **roho** (ufahamu wa Mungu)

Mungu: Utatu wa Mungu, Mungu mmoja aliye Utatu (Baba, mwana na Roho)

Mtu: sehemu tatu ufanya mtu kuwa mtu mmoja (Mwili, nafsi na Roho)

Kuelewa Agano la Kale...

NNE: Adamu kwa ujinga wake aliasi dhidi ya Muumba wake mwenye upendo na akaamua kufuata mapenzi yake. Kwa kujibu uasi wa Adamu (dhambi) Mungu alilaani ardhi kutokana nayo Adamu aliumbwaa na ikasababisha kifo kwa Adamu. ***“Ardhi imelaaniwa kwa ajili yako....Wewe u mavumbi na kwa mavumbi utarudi”*** (Mwanzo 3:17-19).

Kwa hiyo kila mtu hufa kwa sababu sisi (kama vile Adamu) hufanya dhambi.

“Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi... ” (Warumi 5:12).


Kuelewa Agano la Kale...

TANO: Mungu ni mwema kikamilifu na yeye huwakana wote wanaopungukiwa na viwango vyake vikamilifu. Mungu alipeana sheria yake kwa wanadamu ili wajuelililo njema na sawa. Mionganini mwa mambo mengi, sheria ya Mungu inatufundisha hitaji la:

- | | |
|--|--|
| <ol style="list-style-type: none">1. Kamwe usiweke chochote mbele za Mungu.2. Muabudu Mungu na Mungu Peke yake.3. Mpende na umtumikie Mungu na usilidharau jina lake.4. Mheshimu Mungu kama muumba wa vitu vyote na mtoaji wa uzima.5. Tutii na kuheshimu wazazi aliotupa Mungu. | <ol style="list-style-type: none">6. Usimdhuru mtu yeyote kwa njia yoyote.7. Kuwa safi kimapenzi na uwe mwaminifu kwa mwenzio.8. Usiibe.9. Sema ukweli kila wakati.10. Shukuru kwa chochote ulicho nacho na usiwe na vivu. |
|--|--|

Understanding the Old Testament...


SITA: Mungu anapotupima kwenye mizani ya sheria yake kamilifu, mwenendo wetu unakosa kulingana na amri zake.



“...Umelepimwa kwenye mizani nawe umeonekana kama umepunguka” (Danieli 5:27).

Kuelewa Agano la Kale...

SABA: WOTE watendao dhambi (wanakosa kutii sheria na kusawazisha mizani) wanakataliwa mbali nakulaaniwa na Mungu.



“...Nafsi itendayo dhambi itakufa” (Ezekiel 18:4).

Kuelewa Agano la Kale...

NANE: Licha ya dhambi zetu, Mungu bado alitupenda, na hivyo aliahidi kufanya jambo la ajabu: Aliahidi siku moja atatuma "Mwokozi", ambaye atachukua dhambi zetu, kushinda kifo chetu, na kutufanya tukubalike kwa Mungu!

Likinena kuhusu
huyu mwokozi
Agano la Kale
lilitabiri...

*"Utakuwa na kutuhurumia.
Utakanyaga maovu yetu. Nawe
utazitupa dhambi zao zote
katika vilindi vya bahari"*
(Mika 7:19).

Kuelewa Agano la Kale...

Mnamo 712 KK, Agano la Kale lilisema kwamba Mwokozi huyu mwenye upendo angetuokoa kutoka kwa dhambi zetu, kwa kuchukua dhambi zetu juu yake na kuibeba adhabu ya dhambi zetu kwa niaba yetu.

“.....Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote” (Isaya 53:6).



Dhambi




Mwokozi

*“... nafsi itendayo
dhambi itakufa”*
(Ezekieli 18:4).

Kuelewa Agano la Kale...

Ingawa Mwokozi huyu wa ajabu angekufa kwa ajili ya dhambi zetu, Yeye mwenyewe hangekuwa na hatia. Mungu alisema kwamba Mwokozi angetii sheria zake kikamilifu, lakini angevumilia kikamilifu adhabu hiyo kwa niaba yetu.



“Ingawa hana hatia atawafanya wengi kuwa wenye hakinaye atachukua maovu yao, ili wengi wao wasiwe na hatia” (Isaya 53:11-CEV).

Kuelewa Agano la Kale...

Hadi siku hiyo maalum
ilipofika, wakati dhambi za
watu zingewekwa juu ya
Mwokozialiyeahidiwa, Mungu
aliwaamuru watu wake kuweka
dhambi zao kwa **wanyama**
wasio na hatia badala yake.



*“Ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai na
kuungama juu yake uovu wote wa wana wa Israeli, na makosa yao, naam
dhaambi zao zote naye ataziweka juu ya kichwa chake Yule mbuzi”*
(Mambo va Walawi 16:21).

Kuelewa Agano la Kale...


Kuwa na dhambi zao mfano
uliwekwa kwenye wanyama
wasio na hatia, **wanyama**
hao (kwa mfano kondoo,
mbuzi) walihukumiwa kifo
(walitolewa dhabihu), nao
wakatokwa na damu na kufa
badala ya wenyе dhambi.



***“... Uhai wa mwili u katika hiyo damu, nami nimewapa
ninyi hiyo damu juu ya madhabahu, ili upatanisho kwa
ajili ya nafsi zenu”*** (Mambo ya Walawi 17:11).

Kuelewa Agano la Kale...

Kwa kurudi, Mungu alikubali "kutokuwa na hatia" kwa wanyama hawa kama **kifuniko** (upatanisho) kwa watu wenye hatia. Kwa sababu ya upatanisho (kufunika) Mungu angeweza kuwatazama watu hawa wenye hatia na kuona kutokuwa na hatia.



“... Itakubaliwa kwa ajili yake ili kufanya upatanisho kwa ajili yake” (Mambo ya Walawi 1:4).

Kuelewa Agano la Kale...

Dhabihu za **wanyama** zilikuwa
picha ya malipo ya baadaye ya
Mungu kwa dhambi.

Mungu angekubali kwa muda
kifo na kutokuwa na hatiayao
mpaka kifo na kutokuwa na
hatia ya **Mwokozi** iletemalipo
ya kweli na upatanisho wa
dhambi zetu.

MNYAMA =

PICHA
(Alama)

MWOKOZI =

MALIPO
(Vitu)

*“Kwa maana haiwezekani kwa
damu ya mafahali na mbuzi
kuondoa dhambi”* (Waibrania 10: 4).

Lakini Mwokozi huyu anaweza kuwa nani?

Ni mtu gani anayeweza kutii kikamilifu sheria ya Mungu?

Na ni nani angeweza kutupenda vya kutosha kubebadhambi zetu na kufa badala yetu?

MUNGU angeweza! Ndio, Mungu Mwana angezaliwa kama mwanadamu, kwa hivyo angeishi maisha yasiyokuwa na dhambi kwa ajili yetu kisha afe kama mwenye dhambi badala yetu!

“Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto wa kiume; na serikali itakuwa begani mwake; na jina lake litaitwa Mshauri wa Ajabu, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa Amani” (Isaya 9:6).

Kuelewa Agano la Kale...

Mwisho wa Agano la Kale (430 KK), Mungu aliwaambia watu wake kwamba, kabla ya Mwokozi aliyeahidiwa kuja, atatuma kwanza mjumbe maalum ili kuwaandaa watu kwakuja kwake duniani.

***“Tazama, nitamtuma mjumbe wangu, naye
atatengeneza njia mbele yangu...”*** (Malaki 3:1).

Halafu... watu walingojea Mwokozi (na mtume) aje.



NA MWOKOZI AKAJA!

Miaka 400 baadaye, bikira Maria alipata mimba ya Mwokozi kimiujiza. Kuzaliwa kwake kulitangazwa kwa ulimwengu na kumbukumbu zikaandikwa katika Agano Jipywa kwa ajili yetu.

“Naye atazaa mtoto wa kiume, nawe utamwita jina lake YESU, maana, ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka kwa dhambi zao” (Mathayo 1:21).

“Na malaika akawaambia... Ninawaletea habari nje-ma ya furaha kuu ... Kwa maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa Mwokozi, ndiye Kristo Bwana” (Luka 2:10- 11).

Mjumbe Maalum - Yohana Mbatizaji

Yohana Mbatizaji
(Mjumbe maalum)
alikuja mara moja mbele
ya Yesu kuonya juu ya
hukumu ya Mungu ya
siku zijazo juu ya
dhambi na kuwaambia
wote ambao
walitakamsamaha wa
Mungu kwamba
Mwokozi anakuja hivi
karibuni.

Yohana alielezea kwamba dhabihu za
wanyama katika Agano la Kale
zilikuwa tu picha ya Mwokozi, ambaye,
kama mwana-kondoo aliyetolewa
dhabihu, atakuwa upatanisho wa kweli
wa dhambi.

***"Siku iliyofuata Yohana akamwona
Yesu... na kusema," Tazama Mwana-
Kondoo wa Mungu, aichukuaye
dhambi ya ulimwengu! "*** (Yohana
1:29).

Kwa nini Agano la Kale na Jipy?

"Agano" hutoa kitu mtu anapokufa. Ndiyo sababu, tunapotoa wasia, tunasema:

"Huu ni wasia wangu wa mwisho na **agano**."

AGANO LA KALE: Msamaha unaodaiwa na kifo cha wanyama.

“... Kwa maana ni damu inayofanya upatanisho kwa nafsi”
(Mambo ya Walawi 17:11).

AGANO JIPYA: Msamaha uliolipwa kamili na kifo cha Yesu.

Yesu alilieleza hili kama, **“... agano jipy katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu”** (Luka 22:20).

YESU - MBADALA WETU MKUU

Yesu alizaliwa kama mbadala wetu. Maisha ya wanyama hayangeweza kuchukua nafasi ya wanadamu, lakini YESU, **kama mwanadamu**, aliishi kutii amri kamili za Mungu kwa niaba **yetu**.

Biblia inasema Yesu “*... alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi*” (Waembrania 4:15).

YESU ALIFANYA HIVI...

Kwa hivyo ungeweza kupata sifa kwa maisha **YAKE!**

YESU - MBADALA WETU MKUU

Ndipo Yesu alikufa kama mbadala wetu. Vifo vyā wanya-ma hao havingeweza kulipa adhabu kwa wanadamu, lakini YESU, **kama mwanadamu**, alikufa kulipa adhabu ya dhambi kwa niaba **yetu**.

Biblia inasema Mungu alitupenda sana hivi kwamba
“...tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufakwa ajili yetu” (Warumi 5:8).

YESU ALIFANYA HIVI...

Kwa hivyo **ungeweza** kupata sifa kwa kifo **chake!**

YESU - ALIKATALIWA NA KUHUKUMIWA

Ingawa wengi walimwamini na kumpokea Yesu, watu wengi walimkataa na wakamhukumu kifo kwa kusulubiwana warumi.

“Akauchukua msalaba wake akatoka akaenda mahali paitwapo fuvu la kichwa, iitwayo kwa Kiebrania Golgotha: Ambapo walimsulubisha” (Yohana 19:17-18).

Kukataliwa kwa Yesu kulitabiriwa katika Agano la Kale:

“Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu ... ”
(Isaya 53:3).

YESU - ASULIBIWA MSALABANI


Lakini Mungu angetumia **kifo cha Yesu Msalabani** ili kuleta upatanisho mkuu wa dhambi aliyokuwa ameahidi!



*“Kwa maana yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi
kwa ajili yetu; ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika
yeye” (2 Wakorintho 5:21).*

YESU - ASULIBIWA MSALABANI

Msalaba ndio msingi
hatua ya wokovu wetu,
kwa sababukifo cha Yesu
Msalabani kilisawazisha
mizani kikamilifu.



Mungu Baba alimtuma Mungu Mwana kuishi maisha ka-mili kwa ajili yetu na kufa kwa ajili ya dhambi zetu msal-abani. Kwa kuwa mtiifu, na kufa kwa dhambi zetu, Yesu alitimiza kila hitaji la sheria ya Mungu: Alivumilia adhabuya sheria - kifo, na alitiisheria kubwa — ***“Mpende BwanaMungu wako kwa moyo wako wote... na jirani yako kama wewe mwenyewe”*** (Luka 10:27).

YESU - ALIZIKWA NA KUFUFUKA TENA

Baada ya Yesu kufa, yeye pia alizikwa (kama mmoja wetu). Lakini, siku ya tatu, **Yesu alifufuka kutoka kwa wafu** akashinda kifo kwa niaba yetu na kutupatia tumainizaidi ya kaburi!



"Hayupo hapa,

*lakini
amefufuka..."*
(Luka 24:6)

**“... Parapanda italia, na wafu watafufuliwa wasiwe na
uharibifu, nasi tutabadilishwa”** (1 Wakor 15:52).


YESU – YUAJA TENA

Siku moja Yesu atakuja tena kuhukumu ulimwengu, na Mungu sasa anataka watu wote wajiandae kwa hukumuhiyo, kwa kugeuza miyo yao kuelekea kwa Mungu na kumpokea Yesu.

Bibilia inasema Mungu “... *sasa anawaamuru watu wote kila mahali watubu: Kwa sababu ameweke siku, ambayo atakayowahukumu walimwengu kwa haki kwa huyo mtu aliyemchagua; Naye amewapa watu wote uhakikisho juu ya mambo haya, kwa kuwa alimfufua kutoka kwa wafu*” (Matendo 17:30-31).

DINI ZA ULIMWENGU

Dini zote za ulimwengu zina kitu kimoja sawa: Kwa namnamoja au nyingine, zote **zinakuweka** kwa mizani:




Lakini **Injili** (Habari Njema) ni kwamba: **Msalaba umetufungulia njia** ya kukubaliwa na Mungu kwa sifa ya Mwanawe - YESU!




UTAHUKUMIWAJE?

Katika **DHAMBI**
yako?



Au

Katika **HAKI YA Yesu?**



UAMUZI NI WAKO

WOKOVU WA YESU NI ZAWADI YA BURE

Wokovu ambao Yesu alikamilisha kwa ajili yako ni **zawadi ya bure**.

“... Mshahara wa dhambi ni mauti, lakini karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu” (Warumi 6:23).

Huwezi fanya kazi kupata zawadi ya Mungu; na huwezi fanya kazi ya kuitunza. Msalaba ulikuwa kazi ya Yesu, sio yako.

“Kwa maana mmeokolewa kwa neema kwa njia ya imani, na hiyo haitokani na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu, si ya matendo, mtu awaye yote asije akajisifu” (Waefeso 2:8-9).

JE, UTAPOKEA ZAWADI YA MUNGU?

Mungu amemtoa YESU ili dhambi zako **zisamehewe**, nauhusiano wako naye uweze **kurejeshwa**.

Je! Utaamini habari hii njema na kumkubali YESU kama Bwana na Mwokozi wako leo? Je! Utatambua dhambi yako, na kuamini (kuamini) kazi ya YESU kwa ajili yako msalabani, ili uweze kuhukumiwa kwa sifa ya Yesu (Mwana wa Mungu)? Biblia inasema...

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16).

IWAPO NIMKATAE YESU?

Rahisi sana, ukimkataa Yesu, Mungu atakukataa.
Utakufa katika dhambi yako na utakaa milele katika
Ziwala Moto.

Siku ya Hukumu, Biblia inasema Yesu

***“... watakusanya kutoka kwa ufalme wake kila kitu
kinachokwaza, na wale wanaotenda maasi; Naye
atawatupa katika tanuru ya moto; huko kutakuwa na
kilio na kusaga meno”*** (Mathayo 13:41-42).

UCHAGUZI NI WAZI

Wote wanaomtegemea YESU wataokolewa kutoka kwa hukumu ya milele ya Mungu juu ya dhambi, lakini wale am-bao hawamwamini kama Mwokozi wao watahukumiwa.

***“Amwaminiye yeye hahukumiwi, lakini asiyemwamini
amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuliamini
jinala Mwana wa pekee wa Mungu ... ”*** (Yohana 3:18).

UAMUZI WAKO NI UPI?

Dhambi zako sasa zinakutenga na Mungu, lakini Mungu anakupenda rafiki yangu. Yesu alitoa uhai wake kwa ajili yako. Na, hata ikiwa dhambi zako ni kubwa sana na zinafikajuu kama Mbingu yenyewe, Mungu sasa anasimama na mikono yake imenyooshwa kuelekea kwako, tayari ku- kusamehe ... yuko tayari kukupokea, ikiwa uko tayari kumpokea Mwanawe.

Je! Utampokea sasa?

“Sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii?” (Waibrania 2:3).

TUNATAKA KUKUSAIDIA!

Umepokea zawadi nzuri ya Mungu? Ikiwa umemkubali Yesu kama Mwokozi wako, au ikiwa una maswali, tunataka kusikia kutoka kwako! Tunapenda kujibu maswali, na tuna rasilimali ambazo zinaweza kukusaidia kukua katika imani yako mpya kwa Yesu Kristo.

Mchungaji George Odero, Forward Church-Rongai
Mayor Road No.5, Ongata Rongai

Simu: 0726916133

Barua pepe: forwardchurchke@gmail.com Sanduku la
Barua: 105019-00101, Nairobi, Kenya

Kupambana na uhakikisho? www.knowimsaved.com
nakala zaidi wasiliana na: knowimsaved@gmail.com

Kusoma ujumbe huu itakuchukua dakika 30; umilele utachukua milele. Je! Utatumia dakika 30 kujua jinsi utakavyotumia umilele?

“Kwa maana itamfaidi nini mtu, akiupata ulimwengu wote na kupoteza nafsi yake mwenyewe?” (Mariko 8:36)